**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 25 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

97. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mita ana Idara Maalum za SMZ:

Kwa muda mrefu sasa, Zanzibar ni nchi iliyojikita katika biashara mbali mbali, na eneo la Darajani ni sehemu muhimu kwa kuwasaidia wananchi wetu kuyaimarisha maisha yao kupitia biashara zao katika eneo hilo. Hata hivyo, Serikali yetu ilichukua jukumu la kuwahamisha wafanyabiashara wa eneo hilo na hivi sasa limekuwa likitumika kwa maegesho ya magari na shughuli nyengine.

(a) Je, Serikali ilikuwa na mpango wa kuwaondosha wafanyabiashara hao katika eneo hilo la Darajani.

(b) Je, hivi sasa Serikali ina mpango gani wa kulitumia eneo la biashara la Darajani.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

147. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba Mahkama zinatoa haki, kumekuwa na kudharauliwa kwa maamuzi ya Mahkama kabla au mara tu baada ya Hakimu kuondoka Mahkama husika.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba katika kesi ya ardhi katika kijiji cha Mzambarauni iliyotolewa hukumu katika Mahkama ya Wete, ardhi ilivamiwa tena mara tu baada ya Hakimu husika kuondoka.

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba amri ya polisi ya kukataza na kuwacha uvamizi wa ardhi hiyo ndani ya mwezi mmoja haikutekelezwa.

(c) Je, Serikali inafahamu kwamba, baada ya amri ya polisi ya kukataza uvamizi sambamba na hukumu ya Mahkama ilisababisha kuchukuliwa, kwa amri ya Sheha, aliyeshinda kesi na kupelekwa polisi Wete na hadi sasa hajapata haki yake.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

83. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la unyanyasaji wa wanawake kwa kupigwa na waume zao hadi kupata majeraha makubwa na wengine kufariki.

(a) Katika kukabiliana na hali hii, Serikali haioni haja ya kuanzisha utaratibu wa kijamii wa kuwahifadhi kwa muda maalumu wanaume wanaowapiga wake zao huku hatua nyengine za kisheria zikiendelea.

(b) Je, kuna mpango gani wa kuweka wataalamu wa mambo ya afya ya akili (psychiatrists) ili waweze kuwatibu wanaume wenye tabia za kuwapiga wake zao.

(c) Je, sheria zinaruhusu kwa wanaume wanaowapiga wake zao kuchapwa viboko hadharani ili iwe fundisho kwa wengine.

124. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Suala la upungufu wa madaktari linaonekana ni changamoto kubwa katika vituo vingi vya afya hususan vya vijijini.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha changamoto hiyo ili wananchi waweze kupata huduma bora za afya.

(b) Je, ni mikakati gani iliyowekwa ili kufanikisha mpango huo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

18. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) katika miaka ya nyuma lilikuwa linatangaza mechi mbali mbali za ndani na kimataifa hasa wakati wa enzi za watangazi Makame Abdalla Seti na marehemu Khamis Shaabani, hali ambayo ilileta hamasa kubwa kwa wapenzi wa mchezo huo. Aidha, Shirika hilo liliingia mikataba mingi na mashirika ya utangazaji kwa mfano redio ya kimataifa ya china na Azam TV.

(a) Kwa nini ZBC imeacha utaratibu wa kutangaza mpira hata kwa mechi za ndani.

(b) Kwa vile ZBC inamashirikiano ya kibiashara na Azam TV na kwa kuwa Azam TV wanaonesha ligi kuu ya Tanzania Bara pia kuonyesha mechi za kimataifa kupitia ZBC2 Je, ni kwa nini ZBC isifanye mazungumzo na uongozi wa Azam TV ili ZBC na wao waweze kuonesha mechi hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

143. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kadhia ya kutounganishwa umeme katika sehemu ya Machengwe Kijiji Kipya ambapo kulihitajika nguzo tatu hadi nne kufika barabarani kwenye laini ya umeme na malipo kutoka kwa wananchi yalishafanyika zaidi ya miezi mitano iliyopita na bado huduma haijapatikana.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijawapatia huduma ya umeme wananchi wa Machengwe Kijiji Kipya ndani ya jimbo la Pandani pamoja na kwamba wameshalipia zaidi ya miezi mitano iliyopita.

(b) Je, ni lini Serikali itawapatia huduma ya umeme kama walivyoomba na kuilipia wananchi wa Machengwe Kijiji Kipya ndani ya jimbo la Pandani.

(c) Kwa vile Serikali imetoa miongozo mipya ya bei na gharama kuhusu kuungiwa wananchi huduma ya umeme. Je, ni kiasi gani, lini na kwa utaratibu upi Serikali itarejesha fedha za ziada zilizokwishalipwa na wananchi wa Machengwe Kijiji Kipya ndani ya jimbo la Pandani.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

37. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukuwa jitihada kubwa katika sekta ya usafiri ikiwemo usafiri wa anga. Katika jimbo la Nungwi tayari kipo kiwanja cha ndege na tayari kinatoa huduma.

(a) Je, ni lini huduma ya kuchukua na kupokea abiria itatolewa.

(b) Je, wale waliokuwa na maeneo yaliyojengwa kiwanja hicho watamaliziwa lini kulipwa fidia zao.

53. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea barabara yenye lami katika ubora wa hali ya juu inayotoka Bububu hadi Mkokotoni. Hata hivyo, ndani ya jimbo la Mkwajuni kuna barabara imetoka Mkwajuni mpaka Matemwe ambayo kwa muda mrefu wananchi wameweka matuta ya kifusi ili kupunguza ajali zinazotokea mara kwa mara.

(a) Je, lini Serikali itajenga matuta ya kudumu katika barabara hiyo.

(b) Barabara ya zamani iliyoachwa baada ya kujengwa mpya, ni lini itafanyiwa matengenezo kwa kuwa wananchi bado wanaihitaji na baadhi ya siku barabara mpya hujaa maji.

(c) Je, ni lini Serikali itajitolea kuweka usalama wa matuta na alama za waenda kwa miguu katika eneo la barabara ya Mkwajuni ili kuwasaidia wananchi wanaojitolea kukatisha barabara, wanafunzi na watu wengine wanaotembea kwa miguu.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

117. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na kauli ya Serikali ya kuwataka wafanyabiashara kutopandisha bei za bidhaa kama vile mchele, sukari na mafuta ya kula.

Je, Serikali imechukuwa hatua gani kusimamia suala hili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

131. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kutujengea skuli ya kisasa ya sekondari na msingi katika shehia yetu ya Mwambe, lakini katika skuli ya maandalizi na msingi tunao upungufu mkubwa wa walimu wapatao hamsini.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni tatizo la upungufu wa walimu ni kubwa mno.

(b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa ili kupunguza changamoto hiyo.

## II. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):</u>**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C):</u>**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

| | |
|---|---|
| **Zanzibar,** | **(Raya Issa Msellem)** |
| **25 Februari, 2022.** | **<u>KATIBU WA BARAZA</u>.** |